



The Economic and Social Research Foundation

TAKNET Policy Brief Series No. 013 - 2010

Msongamano wa Magari Jijini Dar es Salaam: Nini Kifanyike?

Mjadala huu uliandaliwa na kuendeshwa na Bw. Biniface Makene

UTANGULIZI

Msongamano wa magari jijini Dar es Salaam unaweza kusimuliwa kwa namna nyingi. Ukweli ni kuwa, kila anayeishi jijini hapa ana maelezo yake kuhusu anavyoathirika na msongamano wa magari. Maeneo sugu ya foleni ni yale ya makutano ya barabara kubwa na sehemu nyingine ni zile ambazo huathirika wakati mvua zikinyesha. Hivi karibuni Rais Jakaya Kikwete alieleza kuwa katika kipindi chake cha pili atahakikisha jiji la Dar es Salaam linapata barabara za juu maarufu kama 'fly-over'.

Kwa mujibu wa Rais Kikwete, barabara hizo zitajengwa katika maeneo ambayo yanakutanisha barabara mbalimbali na maeneo yanayokabiliwa na msongamano mkubwa. Barabara zinazopewa kipaumbele katika ujenzi wa fly-overs ni zile za Mwalimu Nyerere na Morogoro. Lakini hizi bado ni kauli tu ambazo hazijaanza utekelezaji hali

inayofanya kuendelea kumomonyoka kwa uchumi wa taifa na wa mtu mmoja mmoja. Ni jambo la wazi kuwa idadi ya magari inaongezeka kwa kasi jijini hapa, hali hii inaonesha kwamba watu kumiliki magari sio tena kitu cha anasa bali inatokana na uduni wa usafiri wa umma.

Ofisi nyingi za umma zimejengwa eneo moja hali inayowafanya wakazi wa jiji hili kuwa na uelekeo mmoja kila asubuhi na jioni. Barabara za jiji ni za zamani sana hivyo haziendani na kutanuka kwa jiji. Sambamba na hilo, ubora wa miundombinu sio wa kuridhisha hasa wakati wa mvua. Pia kumekuwepo na matatizo ya mipango miji, ambapo huduma zinazofanana hupatikana sehemu moja ikiwa ni pamoja na makazi ya watu wengi kuwa mahala pamoja.

MALENGO YA MJADALA

Mtandao wa TAKNET ulitoa

nafasi kwa umma kujadili kwa kina tatizo la msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam ili kutafuta jawabu au suluhisho la tatizo hili. Zaidi ya hayo, mjadala huu ulitarajiwa kutoa mapendekezo yatakayosaidia kupunguza kama sio kuondoa kabisa adha ya msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam. Mjadala huu ulifanyika kwa zaidi ya miezi miwili ambapo mawazo zaidi ya 60 yalitolewa huku mashuhuda wa hoja hii wakiwa zaidi ya 700.

Wachangiaji wengi wameonyesha kufahamu kwa kina kuhusu tatizo hili la msongamano wa magari jijini Dar es Salaam. Kupitia michango yao wameweza kubainisha mambo ya kufanyika na pia vyanzo vya msongamano wa magari.

SABABU ZA MSONGAMANO

Washiriki wa mjadala walibainisha sababu kadhaa

zinazopelekea kuwepo kwa msongamano mkubwa wa magari katika jiji la Dar es Salaam. Miongoni mwa vyanzo vya msongamano wametaja vifuatavyo: (i) Kutokuwa na barabara za kutosha na zilizopangiliwa vizuri, (ii) Uchakavu wa magari, (iii) Uduni wa huduma za usafiri wa umma, (iv) Kutokuwa na mpango mji unaoeleweka, (v) Ofisi za serikali na huduma nyingine kuwa katika eneo moja, (vi) Kuongezeka kwa idadi ya watu jijini tofauti na miji mingine nchini, (vii) Kutokuwa na mfumo wa kutoa huduma za jamii kwa saa 24 za siku, na (viii) Usimamiaji mbaya wa sheria za barabara.

ATHARI ZITOKANAZO NA MSONGAMANO WA MAGARI

Wachangiaji wa mjadala huu wamebainisha athari zitokanazo na tatizo la msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam. Zipo athari nyingi za kiuchumi, kijamii na kimazingira. Imebainishwa kwamba misongamano ya magari inachangia kwa kiasi kikubwa kuporomosha uchumi wa watu binafsi wa taifa na hata kuendeleza umaskini (Dk. Khamis).

Wananchi wanalazimika kutumia kiasi kikubwa cha mafuta (pesa) kutembea mwendo mfupi. “Angalia muda unaopotea barabarani na petroli/dizeli na mafuta mengine ya kulainisha mitambo inayopotea bure hasa

ukizingatia kwamba vyote hivi tunaagiza nje ya nchi” ni hifadhi ya fedha za kigeni kiasi gani benki kuu inatumia kununulia bidhaa hizi,” alihoji Festo Maro.

Vile vile athari zingine zilizoainishwa ni pamoja na uharibifu wa mazingira kutokana na hewa mkaa inayotolewa na magari yanayotumia muda mrefu njiani yakiwa yananguruma bila kutembea. Vile vile watumiaji wa magari hayo hufika katika sehemu zao za kazi na hata majumbani mwao wakiwa wamechoka na hivyo kutokufanya shughuli zao ipasavyo.

Mawazo mbalimbali yalitolewa juu ya namna ya kukabiliana na msongamano wa magari jijini Dar es Salaam. Vyanzo vya msongamano pia vilitajwa na vinaorodheshwa hapa chini pamoja na mapendekezo ya namana ya kuepuka msongamano.

NAMNA YA KUKABILIANA NA MSONGAMANO

4.1 Ujenzi wa Dar es Salaam mpya

Wachangiaji wengi katika mada hii wanakubaliana na hoja ya ujenzi wa mji mwingine nje ya Dar es Salaam na kuacha mji wa zamani kama ulivyo ili kuhifadhi historia yake kwa vizazi vijavyo. Dk Omari Khamis anasema; “Mji huu mpya ujengwe kwa makini sana ili tuepuke msongamano si

wa magari tu bali hata wa nyumba. Ofisi za serikali zisambazwe na kila eneo liwe na huduma zote za kijamii zinazohitajika katika maisha ya kila siku kwa mfano maduka, hospitali, vituo vya polisi, shule na mahoteli n.k”

Sambamba na wazo hili baadhi ya wachangiaji wanashauri ianzishwe miji midogo midogo (satellite cities) pembezoni mwa jiji la Dar es Salaam ili kupunguza muelekeo wa magari kwenda na kutoka katikati ya jiji. Dhana hii ya ujenzi wa mji mpya, inarejesha wazo la kuhamishia makao makuu ya nchi mjini Dodoma, wazo ambalo limekuwa likisuasua na sababu kubwa ikiwa kukosekana kwa utashi wa dhati kutoka kwa viongozi wetu.

Wachangiaji wamesisitiza kwamba kuhamishia makao makuu ya nchi Dodoma kutasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza msongamano wa magari jijini Dar es Salaam.

4.2 Utanuaji na uboreshaji wa miundombinu

Kwa mujibu wa maoni ya wadau mbalimbali, inaonekana kuwa mbinu hii ni ya muda mfupi. Uboreshaji wa miundombinu yaani njia za maji taka, barabara kuu na zile zinazounganisha mitaa unaweza kufanyika lakini bado tatizo hili la msongamano likaendelea kuwepo baada ya siku chache. Vilevile bado kuna haja ya kujenga barabara za juu

maarufu kama Fly-overs hasa katika makutano ya barabara kuu zenye msongamano mkubwa kama vile Magomeni, Ubungo, Tazara, Morocco n.k.

Wachangiaji wamezishauri Manispaa za jijini kuhakikisha zinakarabati barabara zote zinazounganisha mitaa (ring roads) ili kupunguza msongamano katika barabara kuu. Wameshauri pia matumizi ya miundombinu ya reli iliyopo hasa inayotoka maeneo ya Pugu, stesheni, Tabata na kuishia Mabibo-Ubungo. Kutumika kwa miundombinu hii kutasaidia kupunguza magari yaendayo mjini kwa kuwa reli itamudu kubeba watu wengi kwa wakati mmoja.

Sambamba na hilo, wadau walipendekeza matumizi ya usafiri wa maji kwa kutumia boti hasa kutoka maeneo ya Tegeta, Kunduchi na Msasani kwenda Posta. Njia hii itaweza kupunguza msongamano katika barabara ya Ali Hassan Mwinyi na pia itatanua mji kwa kuwapa fursa wananchi wengi kukaa nje ya jiji na kumudu kufanya kazi mjini pasipo kuwa na hofu ya tabu ya usafiri.

4.3 Utozaji kodi kwa magari yanayoingia mjini

Mchangiaji Nyangubho Nyega anaona; “upo umuhimu wa kudhibiti uingiaji wa magari makubwa kama malori katikati ya mji. Inawezekana tukaweka namba maalum za magari

yanayoruhusiwa kuingia mjini kwa kutazama gari lilisajiliwa kwa kazi ipi. Tena ili kufanikisha jambo hili upo umuhimu wa utanuaji wa huduma ili ziwe hadi usiku.” Vile vile wachangiaji wengine wameafiki wazo la kutoza kodi kubwa ya maegesho ya magari kama njia moja wapo ya kupunguza msongamano wa magari katikati ya mji.

4.4 Uboreshaji wa huduma za usafiri wa umma

Huduma za usafiri wa umma ni tatizo sugu kwa mujibu wa wachangiaji wengi wa mjadala huu. Usafiri wa umma jijini Dar es Salaam licha ya kuwa si wa kiwango kinachotakiwa bali pia unawafanya wananchi kuamua kununua magari hata kama walikuwa hawayapi kipaumbele. Mradi wa mabasi yaendayo kasi unaweza kuwa kianzio lakini pia kunahitajika kuingia kwa serikali na watu binafsi katika kuweka mkakati wa kuongeza mabasi ya abiria yenye viwango, yatakayoendeshwa kwa kufuata ratiba maalum kila sehemu ya jiji, hivyo kuwafanya watumiaji kutopoteza muda mwingi katika vituo na pia kuwapa ahueni ya utumiaji usioathiri kazi zao na hali zao za afya.

MAPENDEKEZO KATIKA UBORESHAJI SERA

Wachangiaji wengi waliotoa maoni yao wanaishauri serikali na taasisi husika kudhibiti viashiria vya kuongezeka

msongamano wa magari kwa kuwa na sheria na kanuni zitakazoangalia mambo kama; Ujenzi wa majumba na ofisi ambazo zitakuwa na maegesho ya magari.

Rahim Kachwamba anafafanua kuwa, kama jambo hili litafanyika, upo uwezekano wa magari kupata maegesho na hivyo kutoegeshwa barabarani hali inayosababisha kufunga baadhi ya barabara jijini hasa nyakati za kazi. Kuzuia mabasi madogo ya abiria kuingia mjini na kuruhusu makubwa tu yenye uwezo wa kubeba abiria kuanzia 50.

Uwepo ukaguzi wa leseni za magari unaotumia vifaa vya kisasa ili kubaini leseni feki, kwa lengo la kuondosha magari chakavu kutumika mjini. Huduma za jamii kama uwanja wa ndege kujengwa nje ya jiji tofauti na sasa ambapo unafanyika utanuaji wake katika eneo ambalo linaonyesha wazi litaongeza msongamano wa magari kuliko kupungua kwake. Ujenzi wa mitaro ya maji ya kutosha ili kurahisisha upitaji wa maji wakati wa mvua.

Kutoza kodi huduma mbalimbali zinazosababisha magari kutembea taratibu kama vile harusi, ili kuongeza vipato kwa manispaa jijini hapa na pia kupunguza foleni zisizo na maana katika baadhi ya maeneo hasa nyakati za siku za mwisho wa wiki. Kuhamishia makao makuu ya nchi Dodoma.

HITIMISHO

Wachangiaji wengi wanaelezea hisia zao kwa serikali wakiamini kuwa hakujafanyika kazi ya ziada hasa ile inayolenga kujenga Dar es Salaam mpya baada ya kutazama athari zilizopo sasa. Tena inaonyeshwa kuwa, majadiliano kati ya wataalamu wanaohusika na kupanga miji sambamba na wananchi hayajafanyika kwa kina hali inayosababisha mipango mingi kubakia katika karatasi ama kukosa vyanzo vya fedha vya kuiendesha.

Kama kutakuwepo mahusiano

chanya kwa wadau wote bila shaka tatatizo hili linaweza kupata ufumbuzi haraka kwa kuwa linagusa maisha ya kila mwananchi anayeishi jijini Dar es Salaam.

Jukumu la kuondoa tatizo hili ni la wabia wote, ikiwa ni pamoja na Serikali kuu na serikali za mitaa, umma kwa ujumla pamoja na taasisi za kiserikali kama vile SUMATRA, Jeshi la polisi na taasisi binafsi. Umma unatakiwa kuzingatia sheria na taratibu za matumizi ya barabara, wamiliki wa vyombo vya usafiri waajiri wafanyakazi wenye sifa na kuhakikisha

vyombo vyao vipo katika hali nzuri na taasisi za kiserikali zipanue miundombinu na zisimamie matumizi mazuri ya miundombinu iliyoipo.

TAKNET inapenda kuwashukuru wafuatao kwa kushiriki kwao katika mjadala huu: Bw. Festo Maro, Bw. Boniphace Makene, Dk. Omari Mwinyi Khamis, Ndg. Nyangubho Nyega, Bw. Jacks Meena, Ndg. Loyori Kisota Laizer, Ndg. Rah Kachwa, Bw. Abdallah Hassan, Ndg. Toroka Mzee, Dr. S. Moyo, Bw. Novatus Kaijage, Bw. Michael Athuman Mpombo, na Ndg R.M. Besha.

Other TAKNET Policy Briefs:

1. Growth and Poverty Reduction in Tanzania: Why such a Mismatch? (Policy Brief number 1)
2. The Role of Information and Communication Technologies (ICT) in Enhancing the Livelihood of the Rural Poor (Policy Brief number 2)
3. Incentive Package for Foreign Direct Investment (FDI) in Tanzania (Policy Brief number 3)
4. Tatizo la Walemavu wa Ngozi (Albino) Tanzania: Nini Kifanyike? (The Plight of Albino in Tanzania) (Policy Brief number 4)
5. Petroleum Policy and Constitutional Paradox in the United Republic of Tanzania (Policy Brief Number 5)
6. Tanzania National Poverty Reduction Framework – MKUKUTA What are the Lessons (Policy Brief number 6)
7. The Effect of Global Financial Crisis and Way Forward for Tanzania (Policy brief number 7)
8. 2009/10 Government Budget: What impact should be expected? (Policy Brief number 8)
9. Social Welfare and Ageing in Tanzania (Policy Brief number 9)
10. Tanzanian Cultural Environment and Economic Growth (Policy Brief number 10)
11. School Competition and Student Learning Rights (Policy Brief number 11)
12. Informal Sector Taxation in Tanzania

For More Information on these series please contact:

The Project Coordinator
Tanzania Knowledge Network
Economic and Social Research Foundation
P.O. Box 31226, Dar es Salaam, Tanzania
E-mail: taknet@esrf.or.tz, Website: www.taknet.or.tz

Join TAKNET be part of these series



Tanzania Knowledge Network (TAKNET) is a joint initiative by the United Nations through its joint Program on Capacity Development for Development Management under one UN initiative, The Government of the United Republic of Tanzania and The Economic and Social Research Foundation (ESRF).

